

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKALA WA NISHATI VIJIJINI (REA)



Energising Rural Transformation

MWONGOZO WA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MKOPO

WA

**UWEZESHAJI WA UJENZI NA UENDESHAJI
WA VITUO VIDOGO VYA BIDHAA ZA MAFUTA
(PETROLI NA DIZELI) VIJJINI**

MACHI, 2024

Umeandaliwa Na:
Jengo la Wakala wa Nishati Vijijini (REA),
Barabara ya Medeli,
S. L. P. 2153,
Dodoma, Tanzania.
Simu .: +255-26 232-3504/6
Barua pepe: info@rea.go.tz
DODOMA, TANZANIA

YALIYOMO

| | |
|---|----|
| YALIYOMO | ii |
| MAANA ZA MANENO | iv |
| DIBAJI..... | v |
| 1. UTANGULIZI | 1 |
| 2. LENGO LA MWONGOZO | 1 |
| 3. MAHITAJI YA KITUO KIDOGO CHA MAFUTA VIJIJINI | 2 |
| 4. VIGEZO VYA UTOAJI MKOPO..... | 2 |
| 4.1 Vigezo vya Kiufundi..... | 2 |
| 4.1.1 Vigezo kwa Mwombaji (Mwendelezaji)..... | 2 |
| 4.1.2 Vigezo Stahili vya Eneo/Mahali | 3 |
| 4.1.3 Vigezo vya ujenzi | 4 |
| 4.2 Vigezo vya Kifedha na Uzoefu wa Biashara kwa Mwombaji | 5 |
| 5. MFUMO WA UTENDAJI WA KILA TAASISI | 5 |
| 5.1 Majukumu ya Taasisi | 6 |
| 5.1.1 Wizara ya Nishati | 6 |
| 5.1.2 Wizara ya Fedha | 6 |
| 5.1.3 Ofisi ya Rais – TAMISEMI..... | 6 |
| 5.1.4 Wakala wa Nishati Vijijini | 6 |
| 5.1.5 Mamlaka ya Udhibiti Wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)..... | 7 |
| 5.1.6 Wakala wa Amana | 7 |
| 5.1.7 Taasisi ya Fedha (Benki)..... | 7 |
| 5.1.8 Benki Kuu ya Tanzania..... | 8 |
| 5.1.9 Halmashauri za Wilaya | 8 |
| 5.1.10 Mwendelezaji wa Mradi | 8 |
| 6. MCHAKATO WA MAOMBI YA MKOPO..... | 9 |
| 6.1 Hatua ya kwanza – Kutangaza fursa ya Mkopo..... | 9 |
| 6.2 Hatua ya Pili – Kuwasilisha maombi ya mkopo..... | 9 |
| 6.3 Hatua ya Tatu – Uchambuzi wa maombi | 9 |
| 6.4 Hatua ya Nne – Uhakiki wa Taarifa za Mwombaji | 9 |
| 6.5 Hatua ya Tano – Maamuzi kwa vigezo vya kiufundi | 9 |
| 6.6 Hatua ya Sita – REA kuwasilisha orodha ya waombaji kwa Benki..... | 9 |
| 6.7 Hatua ya Saba – Benki kufanya tathmini ya kifedha..... | 9 |
| 6.8 Hatua ya Nane - Benki kuwasilisha matokeo ya tathmini ya kifedha .. | 10 |
| 6.9 Hatua ya Tisa – REA kutoa ruhusa kwa Benki kutoa Mikopo | 10 |
| 6.10 Hatua ya Kumi – Benki kutoa mikopo kwa waombaji..... | 10 |
| 7. MASHARTI YA MKOPO..... | 10 |
| 8. UJENZI WA KITUO | 11 |
| 9. UENDESHAJI WA KITUO | 11 |

VIAMBATISHO

| | |
|---|-----|
| Kiambatisho 1 – Mchoro wa kituo kidogo cha mafuta vijijini | 15 |
| Kiambatisho 2 – Mpango wa biashara | 133 |
| Kiambatisho 3 – Mahitaji ya makadirio ya ujenzi wa kituo..... | 15 |
| Kiambatisho 4 - Muonekano wa kituo kidogo cha mafuta vijijini | 16 |
| Kiambatisho 5 – Mfumo wa kutenganisha maji na mafuta..... | 16 |

MAANA ZA MANENO

| | |
|-------------|--|
| BENKI | Taasisi ya Kifedha ya kutoa Mkopo |
| BoT | Benki Kuu ya Tanzania |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| OSHA | Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi |
| REA | Wakala wa Nishati Vijijini |
| REB | Bodi ya Nishati Vijijini |
| REF | Mfuko wa Nishati Vijijini |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANROADS | Wakala wa barabara Tanzania |
| TIN | Namba ya Mlipa Kodi |
| TPDC | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania |
| TZS | Shillingi ya Ki-Tanzania |

DIBAJI

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ulianzishwa kwa Sheria ya Nishati Vijijini, Na 8 ya Mwaka 2005 na kuanza rasmi mwezi Oktoba 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa iliyokuwa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003, Sheria ya Nishati Vijijini pia ilianzisha Bodi ya Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini.

Wakala wa Nishati Vijiji ni Taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Nishati, yenye jukumu la kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya nishati bora kwa lengo la kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi vijijini. Wakala wa Nishati Vijijini kupitia Wizara ya Nishati hufanya kazi kwa kushirikiana na Wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wabia wa Maendeleo.

Katika kuhakikisha nishati bora na salama maeneo ya vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini, umeendelea kutekeleza majukumu yake ambapo kwa kiasi kikubwa amekijikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na mafanikio makubwa yameonekana. Wakala wa Nishati Vijijini pia unatekeleza miradi mbalimbali ya Nishati ya kupikia. Katika kuongeza upatikanaji wa nishati vijijini, Wakala pia unawajibu wa kuhakikisha nishati ya mafuta (petroli na dizeli) inapatikana vijijini kwa uhakika na inakuwa safi na salama.

Serikali ya Tanzania imedhamiria kutekeleza mpango wa kuwezesha ujenzi wa vituo vipyta vidogo vya gharama nafuu vya bidhaa za mafuta (petroli na dizeli) katika maeneo ya vijijini ili kuondosha njia zisizo salama za uhifadhi wa mafuta hayo ndani ya nyumba yakiwa kwenye mapipa au madumu ya plastiki. Aidha, mpango wa Serikali utaondosha utaratibu uliozoleka vijijini wa kuuza bidhaa hizo kwa kutumia chupa za plastiki jambo ambalo si salama kwa watu na mazingira.

Kwa kutambua hali hiyo na kwa kuzingatia kuwa moja ya malengo ya Sera ya Nishati ya Mwaka 2015 ni kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati na kwa bei nafuu katika maeneo yote ya nchi kwa njia iliyosalama, Wakala wa Nishati Vijijini umeandaa mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa uwezeseshaji wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vipyta vidogo vya mauzo ya petroli na diseli vijijini ili kuhakikisha bidhaa hiyo upatikana kwa uhakika, gharama nafuu na salama kwa watu na mazingira.

Mwongozo huu wa Serikali unalenga kusaidia kupatikana kwa huduma ya mafuta vijijini kwa njia salama na rafiki kwa mazingira kupitia utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa ushirikiano kati ya Wakala wa Nishati Vijijini na

Taasisi ya fedha (Benki). Kupitia mpango huu, mikopo itatolewa kwa kushindanisha waendelezaji wanaokusudia kutoa huduma za mafuta maeneo ya vijijini.

1. UTANGULIZI

Mwongozo wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vidogo vya gharama nafuu vya mafuta vijijini Tanzania Bara unaainisha vigezo kwa mwombaji wa mkopo na matumizi ya Fedha za Mfuko wa Nishati Vijijini kwa ajili ya kutoa mikopo kwa waendelezaji waliokidhi vigezo kwa kazi za ujenzi wa kituo, usimikaji wa mitambo na mtaji wa uendeshaji.

Fedha hizi za mradi ni sehemu ya juhudini za Serikali zinazolenga kuondosha uhifadhi mafuta ndani ya nyumba kwa kutumia mapipa na madumu ya plastiki katika kuhifadhi mafuta ya petroli na dizeli na chupa za plastiki katika kuuza bidhaa hizo hususani kwa watumiaji wadogo kama vile waendesha pikipiki “bodaboda” katika maeneo ya vijijini

Mwongozo wa uendeshaji unaeleza: (i) vigezo kwa mwombaji wa mkopo; (ii) taratibu zinazopaswa kufuatwa na Wakala wa Nishati vijijini katika kuchambua maombi ya mkopo; (iii) taratibu za Benki za kutoa mikopo kwa waombaji (iv) fomu zinazotumika katika mchakato wa maombi, mapitio na uidhinishaji; na (v) majukumu ya watendaji mbalimbali wanaohusika katika kutumia mwongozo huu.

Mwongozo huu utatumika katika kufanya uchambuzi wa maombi ya mikopo kwa waendelezaji wa vituo vipyta vidogo vya mafuta vijijini na utapatikana katika tovuti ya Wakala wa Nishati Vijijini.

Wakala wa Nishati Vijijini atatoa tangazo kwa waombaji kupitia tovuti ya REA (www.rea.go.tz), tovuti ya Wizara ya Nishati, tovuti ya EWURA, tovuti ya Taasisi ya fedha (Benki) na tovuti ya TAMISEMI pamoja na magazeti, televisheni na redio za ndani (Local Radio) zinazotoa huduma Tanzania Bara.

Aidha, mwongozo utafanyiwa mapitio kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha za mradi, mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali pamoja na mrejesho/maoni kutoka kwa wadau wakati wa utekelekezaji wa mradi huu.

2. LENGO LA MWONGOZO

Lengo kuu la mwongozo huu wa utoaji na usimamizi wa mkopo wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vipyta vidogo vya bidhaa za mafuta ya petroli na diseli vijijini ni kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa waendelezaji waliokidhi vigezo vya kupata mkopo wa kujenga na kuendesha vituo vidogo vya mafuta katika maeneo ya vijijini Tanzania Bara. Mwongozo pia unaainisha majukumu ya taasisi husika katika kufanikisha malengo ya Serikali ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi na uendeshaji wa vituo vidogo

vyaneye gharama nafuu maeneo ya vijijini. Utekelezaji wa mpango huu unategemewa kuwa na matokeo muhimu yafuatayo:-

- i. Kutokuwepo kwa matumizi ya mapipa, madumu ya plastiki na chupa za plastiki katika kuhifadhi, kusambaza na kuuza bidhaa za mafuta ya petroli na diseli vijijini;
- ii. Uwepo wa vituo vya mafuta vijijini;
- iii. Uhifadhi wa mazingira na usalama wa jamii na mali zao;
- iv. Upatikanaji wa uhakika wa nishati za petroli na dizeli kwa bei elekezi ya Serikali na kuwapunguzia gharama za usafiri wananchi waishio vijijini;
- v. Kuongeza ajira maeneo ya vijijini;
- vi. Kuongeza upatikanaji wa mafuta bora kwa watumiaji; na
- vii. Ongezeko la mapato ya Serikali.

3. MAHITAJI YA KITUO KIDOGO CHA MAFUTA VIJIJINI

Mradi huu unalenga ujenzi na uendeshaji wa vituo vidogo vya gharama nafuu vya bidhaa za mafuta ya petrol na dizeli vijijini Tanzania Bara na utekelezaji wake utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Fedha hizi za Serikali zitatolewa kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu kwa waendelezaji kupitia benki.

Kituo cha mafuta kitahusisha ujenzi wa tenki la kuhifadhia mafuta la ujazo wa lita 4,500 hadi 5,000 (Underground Storage Tank-UST), Ofisi ndogo (chumba kimoja cha ofisi na vyoo viwili), ufungaji wa pampu ya mafuta moja yenye mikono miwili (dual pump) pamoja na paa lake (canopy) na ujenzi wa mfumo wa kutenganisha mafuta na maji. Kituo kitajengwa ndani ya eneo lisilopungua ukubwa wa mita za mraba 400 (**Kiambatisho Na.1**).

4. VIGEZO VYA UTOAJI MKOPO

Vigezo vya kutoa mkopo wa ujenzi na uendelezaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini vimegawanyika katika makundi mawili; kiufundi na kifedha.

4.1 Vigezo vya Kiufundi

4.1.1 Vigezo kwa Mwombaji (Mwendelezaji)

- i. Awe mtu binafsi, kampuni au vikundi vya wajasiriamali vijijini vilivyosajiliwa na Serikali ya kijiji au Mamlaka husika;
- ii. Awasilishe kwa Wakala wa Nishati Vijijini barua ya maombi ya mkopo wa ujenzi wa vituo/kituo vipya tu na sio vinavyohitaji ukarabati au vilivyoanza kujengwa;

- iii. Awe na vibali vya ujenzi (*construction approvals*) kutoka Halmashauri ya Wilaya au Mji na EWURA au stakabadhi ya malipo ya kibali husika ;
- iv. Awe na barua ya uthibitisho kutoka Halmashauri za Kijiji na Wilaya kuendesha biashara ya kituo cha mafuta katika eneo aliloomba;
- v. Awe na namba ya mlipa kodi (TIN Namba) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania;
- vi. Awe na uthibitisho wa umiliki wa ardhi (Hati miliki ya ardhi, au hati za kimila, au uthibitisho mwingineo wa umiliki wa Ardhi) kutoka kwa halmashauri ya kijiji na Wilaya;
- vii. Awe na barua inayothibitisha mauziano na msambazaji wa mafuta mwenye leseni ya EWURA aliyekaribu kwa ajili ya kununua mafuta; na
- viii. Anapaswa kujaza fomu ya kuonesha namna anavyokusudia kufanya biashara ya mafuta (**Kiambatisho na. 2**).

4.1.2 Vigezo Stahili vya Eneo/Mahali

- i. Kijiji kisicho na kituo cha mafuta;
- ii. Eneo linalopendekezwa kujengwa kituo liwe umbali wa kuanzia kilomita 10 kutoka katika kituo cha mafuta kilicho karibu;
- iii. Eneo linalopendekezwa kujengwa kituo liwe ndani ya barabara zinazosimamiwa na TARURA au barabara za Wilayani zinazosimamiwa na TANROADS umbali wa kuanzia kilomita 7 kutoka kwenye barabara kuu zinazosimamiwa na TANROADS;
- iv. Eneo linalopendekezwa kujengwa kituo liwe linafikika kwa urahisi ;
- v. Eneo linalopendekezwa kujengwa kituo liwe na ukubwa wa angalau mita za mraba 400 ; na
- vi. Eneo linalopendekezwa kujengwa kituo liwe umbali wa mita 50 kutoka kwenye maeneo ya huduma za jamii i.e shule, nyumba za ibada, hospital, masoko, stendi na viwanja vya ndege.

4.1.3 Vigezo vya ujenzi

Kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA (2022) wa ujenzi wa vituo vya mafuta vya gharama nafuu vijijini umeainisha mahitaji ya ujenzi wa kituo (**Kiambatisho Na. 3**), vigezo vya ujenzi wa kituo ni kama ifuatavyo; -

- i. Pampu na sehemu ya kushushia mafuta zinatakiwa kuwa angalau umbali wa mita 4.5 kutoka kwenye mpaka wa kiwanja; kama ilivyoonyeshwa kwenye michoro (site plan);
- ii. Pampu iwe na umbali wa mita 8 kutoka kwenye kifaa chochote kinachoweza kusababisha moto na umbali wa mita 10 kutoka kwenye nyaya za umeme za msongo mkubwa wa kilovolt 33;
- iii. Pampu za mafuta pamoja na sehemu ya kushushia mafuta zinapaswa kuwa angalau umbali wa mita 30 kutoka katika jengo lolote la makazi;
- iv. Matumizi ya bomba za chuma za inchi nne (4) na urefu wa mita tano (5) kwa ajili ya kujengea paa (canopy) lenye urefu wa mita saba (7) na upana wa mita tatu (3). Bomba za inchi moja (1) au inchi moja na nusu (1.5) na bati kwa ajili ya paa;
- v. Matenki ya kuhifadhia mafuta la ujazo wa lita 4,500 hadi 5,000 (Underground Storage Tank-UST) yanatakiwa kufukiwa chini ya ardhi;
- vi. Matenki yapakwe rangi ya kuzuia kutu (Antirust paint);
- vii. Kituo kinatakiwa kisakafiwe kwa zege lenye unene wa inchi sita (6). Eneo mahsusil la kusakafia ni eneo linalozunguka pampu na eneo la kushushia mafuta. Eneo linalozunguka pampu liwe na ukubwa wa angalau mita za mraba 21 (yaani upana mita 3 na urefu mita 7).
- viii. Eneo la kushushia mafuta linatakiwa liwe na ukubwa wa angalau mita za mraba 16 (yaani upana mita 4 na urefu mita 4) ili gari la mafuta liweze kusimama kwenye zege hiyo wakati wa kushusha mafuta (**kiambatisho na. 4**); na
- ix. Eneo linalozunguka pampu na eneo la kushushia mafuta lijengwe mitaro inayoelekea kwenda kwenye chemba ya kuchuja mafuta na maji (Oil/water separator). Chemba ya kuchuja mafuta na maji iwe na vyumba vitatu. Kila chumba kiwe na urefu wa mita moja (1), upana mita mbili (2) na kina mita moja (1). Chemba ifunikwe na mifuniko iliyotengenezwa


na bati au kichanja imara kilichotegenezwa na nondo. Usitumie zege, ili iwe rahisi wakati wa kusafisha. (**kiambatisho na.5**).

4.2 Vigezo vya Kifedha na Uzoefu wa Biashara kwa Mwombaji

- i. Barua ya mwombaji inayoainisha kiasi cha mkopo, lengo la mkopo, chanzo cha fedha za marejesho na mpango wa marejesho na dhamana ya mkopo;
- ii. Awe na uzoefu wa biashara. Kwa waombaji wenye uzoefu wa kuuza mafuta, awasilishe kumbukumbu za mauzo ya mafuta. Mwombaji asiye na uzoefu wa kuuza mafuta, uzoefu kwenye biashara nyingine ye yeyote anayoifanya utazingatiwa;
- iii. Kikundi kiwe na barua kutoka mamlaka husika (Serikali ya Kijiji na mamlaka zilizowasajili) zinazoonyesha madeni na uwezo wao wa kukopa;
- iv. Dhamana ya mikopo ya ujenzi wa kituo kidogo cha mafuta vijiji ni: mali zote za mradi (eneo la mradi, majengo, Vifaa vya mradi, na mafuta), na fedha za mauzo ya mradi; na
- v. Jumla ya thamani ya mali zote zinazowekwa kama dhamana isipungue 1.25 ya mkopo.

5. MFUMO WA UTENDAJI WA KILA TAASISI

Mfumo wa usimamizi wa utoaji mikopo na utekelezaji wa mradi unahusisha Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini, Wakala wa Amana, Taasisi ya fedha (Benki), Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha. Mfumo wa utendaji wa kila Taasisi ni kama unavyonekana katika **Mchoro Na. 1**



Mchoro Na. 1 – Mfumo wa utendaji wa kila Taasisi

5.1 Majukumu ya Taasisi

5.1.1 Wizara ya Nishati

- i. Kusimamia na kuelekeza Wakala katika kufikia malengo ya mradi;
- ii. Kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi;
- iii. Kushirikisha na kuhamasisha wadau kushiriki katika utekelezaji wa mradi pamoja na kuhakikisha upatikanaji bidhaa za mafuta ya petroli na dizeli salama vijijini; na
- iv. Kuweka mazingira wezeshi ya kisera kwa waendelezaji wa vituo vidogo vya bidhaa za mafuta ya petroli na dizeli vijijini.

5.1.2 Wizara ya Fedha

- i. Kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi; na
- ii. Kuidhinisha na kutoa fedha za utekelezaji wa mradi kulingana na mahitaji yaliyowasilishwa.

5.1.3 Ofisi ya Rais – TAMISEMI

- i. Kuhamasisha utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuanzisha vituo vidogo vipyta vya mafuta vijijini kupitia wa Sera ya Maendeleo Mijini na Vijijini na Upelekaji wa Madaraka kwa Umma;
- ii. Kuhakikisha Tawala za Mikoa na Halmashauri zinatimiza wajibu wake katika kutekeleza mpango husika; na
- iii. Kusimamia utendaji wa Mashirika, Taasisi, Programu na miradi iliyo chini ya OR-TAMISEMI

5.1.4 Wakala wa Nishati Vijijini

- i. Kuhamasisha soko, kutoa taarifa muhimu na taratibu kwa waendelezaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini;
- ii. Kuandaa na kusaini mkataba na benki kwa ajili ya kutoa mikopo kwa waendelezaji;
- iii. Kuratibu taratibu za kifedha zinazohusu mradi;
- iv. Kushirikiana na Benki kuchukua hatua endapo mwendelezaji atashindwa kurejesha mkopo kwa kuzingatia masharti ya mkopo kati ya benki na mwendelezaji;

- v. Kuratibu, kusimamia na kufuutilia utekelezaji wa mradi na kutoa taarifa ipasavyo katika mamlaka mbalimbali;
- vi. Kuhakikisha mwongozo unazingatiwa na wadau katika hatua zote za utoaji, usimamizi wa mkopo na utekelezaji wa mradi;
- vii. Kufanya uchambuzi wa kiufundi wa maombi yaliyowasilishwa na waendelezaji;
- viii. Kushughulikia changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi;
- ix. Kufanya mapitio ya taarifa zilizowasilishwa na benki pamoja na waendelezaji; na
- x. Kufanya ufuutiliaji na tathmini ya maendeleo ya mradi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

5.1.5 Mamlaka ya Udhibiti Wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Kuhakikisha vituo vinavyolengwa na mwongozo huu vinaanzishwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo;

5.1.6 Wakala wa Amana

Kufanya ufuutiliaji na tathmini ya maendeleo ya Mradi na kuwasilisha taarifa kwa Wakala wa Nishati Vijijini.

5.1.7 Taasisi ya Fedha (Benki)

- i. Kusaini mkataba na Wakala wa Nishati Vijijini kwa ajili ya kutoa mikopo kwa waendelezaji;
- ii. Kuhakiki uchambuzi wa kiufundi wa mradi uliowasilishwa na Wakala wa Nishati Vijijini.
- iii. Kusimamia matumizi ya fedha za mkopo pamoja na usimamizi wa mradi;
- iv. Kufungua akaunti maalumu ya mradi kwa ajili ya kutoa mkopo na kupokea marejesho;
- v. Kufanya uchambuzi wa kifedha wa maombi ya mkopo;
- vi. Kusaini mikataba ya mkopo na waendelezaji;
- vii. Kutoa mikopo kwa waendelezaji kama ilivyoelekezwa katika mwongozo;

- viii. Kufuutilia na kukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa waendelezaji na kuwasilisha katika akaunti ya Wakala iliyopo BoT;
- ix. Kutunza kumbukumbu za mwenendo wa mkopo; na
- x. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya mradi kwa Wakala kila robo mwakaikijumuisha maendeleo ya Mradi, urejeshaji wa mikopo, mafanikio na matokeo ya mradi.

5.1.8 Benki Kuu ya Tanzania

Kuhamisha fedha kutoka akaunti ya REA iliyopo BOT kwenda akaunti ya Wakala;

5.1.9 Halmashauri za Wilaya

- i. Kutoa kibali cha ujenzi;
- ii. Kutoa kibali cha matumizi ya ardhi;
- iii. Kutoa leseni ya biashara; na
- iv. Kutoa hati milki au uthibitisho wa umiliki wa ardhi.

5.1.10 Mwendelezaji wa Mradi

- i. Kutuma maombi ya mkopo kulingana na tangazo;
- ii. Kuwasilisha taarifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Mwongozo huu na masharti mengineyo ya mkopo;
- iii. Kusaini mikataba ya mkopo na Benki;
- iv. Kurejesha mkopo kwa mujibu wa masharti;
- v. Kutoa taarifa za utekelezaji wa mradi na uendeshaji wa biashara kwa REA na Benki kila mwezi kwa kuzingatia mwongozo “template” utakaotolewa na REA; na
- vi. Kufuata sheria na taratibu zote zinazohusiana na uendeshaji wa biashara ya vituo vyta mafuta.

6. MCHAKATO WA MAOMBI YA MKOPO

Mchakato wa kutoa mkopo umegawanyika katika hatua zifuatazo;

6.1 Hatua ya kwanza – Kutangaza fursa ya Mkopo

Tangazo la fursa kwa wadau litatolewa na Wakala wa Nishati Vijijini kupitia tovuti ya REA (www.rea.go.tz), tovuti ya Wizara ya Nishati, tovuti ya EWURA, tovuti ya Taasisi ya fedha (Benki) na tovuti ya TAMISEMI pamoja na magazeti, televisheni na redio za ndani (Local Radio).

6.2 Hatua ya Pili – Kuwasilisha maombi ya mkopo

Maombi ya mkopo yatawasilishwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini kwa kujaza fomu (**Kiambatisho na. 2**) pamoja na viambatisho viliyoanishwa katika **Kifungu Na. 5.1**

6.3 Hatua ya Tatu – Uchambuzi wa maombi

Wakala wa Nishati vijijini atafanya uchambuzi wa kiufundi wa maombi ya mkopo kwa mujibu wa vigezo viliyoanishwa katika mwongozo huu au tangazo husika.

6.4 Hatua ya Nne – Uhakiki wa Taarifa za Mwombaji

Waombaji wa mkopo waliokidhi matakwa watafanyiwa uhakiki wa taarifa zao na Wakala kabla ya kutolewa kwa matokeo ya uchambuzi kwa waombaji.

6.5 Hatua ya Tano – Maamuzi kwa vigezo vya kiufundi

Wakala wa Nishati Vijijini utaidhinisha na kuandaa orodha ya waombaji waliokidhi vigezo vya kiufundi ikianisha taarifa mbalimbali zikiwemo, jina la mwombaji, kiwango cha mkopo alichoomba, anuani ya mwombaji na eneo la ujenzi wa kituo.

6.6 Hatua ya Sita – REA kuwasilisha orodha ya waombaji kwa Benki

Orodha ya waombaji waliokidhi vigezo vya kiufundi itawasilishwa Benki kuendelea na tathmini ya kifedha kwa mujibu wa Mwongozo.

6.7 Hatua ya Saba – Benki kufanya tathmini ya kifedha

Benki watafanya tathmini ya maombi ya mkopo kwa kuzingatia vigezo viliyoanishwa katika **kifungu cha 5.2**.

6.8 Hatua ya Nane - Benki kuwasilisha matokeo ya tathmini ya kifedha

Benki itawasilisha taarifa ya matokeo ya tathmini ya kifedha ya mkopo kwa REA ikianisha taarifa mbalimbali zikiwemo jina la mwombaji na kiwango cha mkopo kilichoombwa na kilichoidhinishwa na sababu ya kuidhinisha na kutoidhinisha mkopo.

6.9 Hatua ya Tisa – REA kutoa ruhusa kwa Benki kutoa Mikopo

REA itatoa ruhusa kwa Benki kuendelea na taratibu za kutoa mikopo kwa waombaji waliokidhi vigezo baada ya kupokea taarifa ya matokeo ya tathmini. Aidha, REA itamjulisha kila mwombaji matokeo ya maombi yake.

6.10 Hatua ya Kumi – Benki kutoa mikopo kwa waombaji

Benki itatoa mikopo kwa waendelezaji waliokidhi vigezo vyta kiufundi na kifedha. Hatua za kukamilisha mkopo ni kama ifuatayo;

- a) Mwombaji atapewa barua ya kukubaliwa mkopo;
- b) Mwombaji kusaini kukubali masharti ya mkopo;
- c) Benki kusajili dhamana ya mkopo katika Taasisi husika; na
- d) Benki kutoa mkopo kwa mwendelezaji kwa awamu tatu kama ifuatavyo baada ya kukamilisha vigezo vyote vilivyoainishwa kwenye mkataba;
 - i. **Awamu ya kwanza;** itatolewa kwa manunuzi na kazi za ujenzi wa miundombinu (civil works) pamoja na uundaji wa matenki ya kuhifadhi mafuta;
 - ii. **Awamu ya pili;** itatolewa kwa manunuzi na kazi za usimikaji wa mitambo (Mechanical works) pamoja na kumaliza kazi za ujenzi zinazohusiana na awamu hii; na
 - iii. **Awamu ya tatu;** itatolewa kwa ajili ya mtaji wa awali wa kuendeshea biashara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha mafuta na kupatikana kwa leseni ya biashara ya mafuta kutolewa na mamlaka husika.

Maombi ya mwendelezaji sharti yaoneshe mchanganuo wa mahitaji ya fedha katika awamu tatu zilizobainishwa hapo juu. Aidha, utoaji wa fedha kwa awamu inayofuata utazingatia kukamilika kwa kazi za awamu iliyotangulia.

7. MASHARTI YA MKOPO

Pamoja na Masharti ya mkopo kati ya Mkopaji na Benki pia masharti mengine ni kama ifuatavyo;

- i. Mwendelezaji wa mradi hatatakiwa kuuza au kubadili umiliki wa kituo kwa kipindi chote cha marejesho ya mkopo bila idhini ya Benki;

- ii. Mwombaji wa mkopo hataruhusiwa kuomba mkopo wa ujenzi wa kituo zaidi ya kimoja;
- iii. Riba ya mkopo itakuwa asilimia tano (5%) mpaka saba (7%). Kwa sasa tutaanza na asilimia tano (5%) kwa mwaka kwa kipindi cha mkopo. Aidha, kiwango hiki kinaweza kubadilika ili kuhakikisha thamani ya fedha inayotolewa kama mkopo inalindwa;
- iv. Mkopaji atapewa muda wa matazamio usiozidi miezi sita (6);
- v. Marejesho ya mkopo yatafanyika kila mwezi;
- vi. Kiwango cha mwisho cha mkopo kinategemea mahitaji ya mkopaji, kiwango cha juu cha mkopo ni shilingi Milioni Sabini na Tano tu (Sh.75,000,000.00);
- vii. Uthibitisho wa mwombaji kukubali kulipa bima ya majanga ya moto endapo maombi yake yatakidhi vigezo vyote vyta mkopo; na
- viii. Muda wa mwisho wa kurejesha mkopo ni miaka saba (7) ambapo mwombaji anaruhusiwa kurejesha mkopo chini ya kipindi kilichowekwa;

8. UJENZI WA KITUO

Mradi utatekelezwa na mwendelezaji na utaanza baada ya kupata malipo ya awamu ya kwanza ambapo shughuli za ujenzi wa kituo zitaanza rasmi na kukamilika kwa muda usiozidi miezi sita (6). Ujenzi wa kituo utazingatia mwongozo wa ujenzi wa vituo vidogo vyta mafuta kutoka EWURA ambao unaainisha vigezo vyta ujenzi, vigezo vyta maeneo pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi wa kituo. Mchoro wa kituo unaonekana kwenye **kiambatisho Na. 2**

9. UENDESHAJI WA KITUO

9.1 Taratibu za uendeshaji wa kituo

Mwendelezaji wa mradi atawajibika na uendeshaji wa kituo ikiwa ni pamoja na kughamaria shughuli za uendeshaji na utunzaji wa mazingira pamoja na taratibu nyingine kama zilivyoanishwa katika leseni ya uendeshaji wa kituo.


9.2 Utunzaji wa Taratibu za Utunzaji wa Mazingira na Usalaama wa Jamii

Mwendelezaji atatakiwa kuzingatia taratibu za utunzaji wa mazingira na kuhakikisha usalama wa jamii inayozunguka kituo kwa kipindi chote cha kutekeleza mradi.

9.3 Taratibu za kurejesha mkopo

Mwendelezaji wa mradi atatakiwa kurejesha mkopo wote ndani ya miaka saba (7) kwa kuzingatia masharti ya mkopo kati ya mkopaji na Benki. Marejesho yataanza kufanyika baada ya kipindi cha matazamio (grace period). Mwendelezaji wa mradi atafanya marejesho kwa kuzingatia masharti ya mkopo. Marejesho yote ya mkopo yatawekwa kwenye akaunti ya mradi iliyopo katika Benki itakayotoa mkopo. Benki itahamisha fedha hizo kwenda kwenye akaunti ya REA iliyopo BOT kwa kuzingatia masharti ya mkataba.

Kiambatisho 1 - Mchoro wa kituo kidogo cha mafuta vijijini



Kiambatisho 2 - Mpango wa Biashara kwa Waendelezaji

1. Jina la Muendelezaji:
2. Jina La Mradi:
3. Eneo la Mradi:
4. Tarehe ya kuanza ujenzi
5. Tarehe ya kukamilisha ujenzi
6. Aina ya Huduma (Petroli au Diseli au vyote)
7. Gharama ya mradi
8. Kiasi cha Mkopo
9. Tarehe kukopa:
10. Muda wa Mkopo
11. Tarehe ya kuanza Biashara
12. Kiasi cha mauzo (lita) kwa Mwezi
13. Gharama za Uendeshaji:

14. Tarehe ya marejesho ya kwanza ya mkopo:

15. Dhamana ya mradi

16. Kuwepo kwa uhitaji wa huduma ya kituo cha mafuta ndani ya eneo hilo.

17. Mwombaji awasilishe taarifa za kibashara (idadi ya vyombo vinavyotumia mafuta katika eneo husika, bei za mafuta katika eneo husika)

| |
|--|
| |
| |
| |
| |

Kiambatisho 3 - Makadirio ya mahitaji ya ujenzi wa kituo cha mafuta Vijiji

| Na | Kipengele | Maelezo mafupi ya kazi | Idadi | Gharama |
|-----------|--|---|--------------|----------------|
| 1 | Jengo la Ofisi | Mita za mraba 16 (4mx4m); Bati geji 28; tofali za kuchoma au sementi; vyoo viwili (2), sakafu ya sementi, Milango, Madirisha na rangi. | 1 | |
| 2. | Paa la kituo cha mafuta (canopy) | <ul style="list-style-type: none"> Mita za mraba 21 (7mx 3m), Bati la geji 28; paa la chuma lililosimikwa kwenye kitako cha zege; Kitako kijengwe kwa sementi na kiwe na eneo la mita 4.5 sqm (3 x 1.5) na kimo cha mita 0.15 | 1 | |
| 3. | Matenki ya kuhifadhi mafuta | Tenki moja (1) la kuhifadha mafuta. Kama utauza aina zaidi ya moja ya mafuta, matenki yaongezekere sawia. Tenki liwe na ujazo wa angalau lita 4,500 au 5,000; Tenki lijengwe kwa kutumia Chuma cha carbon (carbon steel); Tenki lipakwe kemikali ya kuzuia kutu, Tenki lijengwe chini ya ardhi na kusakafiwa juu kwa zege lenye unene wa inchi sita (6). Eneo la kushushia mafuta liwe na ukubwa wa mita za mraba 16; | 1 au 2 | |
| 4 | Mfumo wa kutenganisha mafuta na maji (Oil/Water Separater) | Mfumo wa kutenganisha maji na mafuta uwe na chemba tatu kama ilivoanishwa kwenye kiambatisho Na. 4 | 1 | |
| 5 | Pampu ya mafuta | Pampu ya mafuta ya kawaida yenye mikono miwili (2); | 1 | |
| 6 | Vifaa vya zimamoto na maji safi | Kituo kiwe na Miundombinu ya maji safi na zimamoto kama ilivoanishwa katika mchoro kiambatisho Na. 2 | Seti moja | |
| 7 | Vifaa vya umeme kwenye kituo | Jengo pamoja na kituo kitandazwe mifumo ya umeme kulingana na viwango vya TANESCO | Seti moja | |
| 8 | Vifaa vya usafi wa kituo | Kituo kiwekwe Miundombinu ya usafi wa mazingira (<i>WC and Septic Tank System</i>) | Seti moja | |
| 9 | Vifaa vya uondoaji maji ya mvua | Kituo kiwekwe Miundombinu ya uondoaji maji ya mvua (<i>Storm Water Drainage System</i>) | Seti moja | |

| Na | Kipengele | Maeleo mafupi ya kazi | Idadi | Gharama |
|-------|-----------|-----------------------|-------|---------|
| JUMLA | | | | |

Kiambatisho 4 – Mfano wa muonekano wa kituo kidogo cha mafuta vijiji



Kiambatisho 5 – Mfumo wa kutenganisha maji na mafuta

